

## Kiswahili kama Lugha Changizi: Uchambuzi wa Kifonolojia wa Maneno Yaliyokopeshwa Lugha ya Kikikuyu

P. I. Iribemwangi  
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

### Ikisiri

Ukopaji katika lugha hupelekea kukua kwa lugha inayokopa. Kwa sababu hiyo, ukopaji ni mchakato uendeleo aushi. Kwa hakika, kila lugha ambayo wazungumzaji wake wamewahi kutagusana na wazungumzaji wa lugha nyingine haiwezi kuepuka maneno ya mkopo. Kutokana na masiala haya, tafiti nyingi zimefanywa kuhusu ukopaji na utohozi. Jambo linalodhirika ni kwamba mkazo huwekwa katika lugha pokezi huko lugha changizi ikipuuza. Kiswahili ni mojawapo wa lugha zinazosemwa kukopa sana hadi kuitwa lugha chotara na baadhi ya wasomi. Hata hivyo, jambo ambalo halijatiliwa mkazo ni kwamba Kiswahili nacho kimechangia katika kukuza msamiati wa lugha nyingi duniani. Hii leo, kuna maneno kadhaa ya Kiswahili hata katika lugha zilizosambaa sana kama Kiingereza. Kikikuyu ni mojawapo ya lugha zilizokopa maneno mengi kutoka Kiswahili. Watumizi wa Kiswahili na Kikikuyu wamekuwa na mtagusano hadi mwanzo wa karne iliyopita. Kutokana na hali hiyo, ukopaji unadhihirika. Makala haya yanachanganua mbinu tofauti za kifonolojia zinazotumika katika kutohoa maneno ya Kiswahili yanapoingia katika Kikikuyu. Kwa kuwa Kikikuyu kina lahaja zipatazo tano tofauti, katika kuchunguza maneno hayo, makala makala haya yatachota kutoka kwa lahaja hizo zote. Makala yatumia mwelekeo wa Mshabaha-Chanzo wa Utohozi wa Manenomkopo (Source-Similarity Model of Loanwords Adaptation) ambao ni mmojawapo wa mielekeo ya Nadharia ya Ulinganifu (Correspondence Theory). Mwelekeo huu husisistiza kuwepo kwa mshabaha/ulinganifu mkubwa baina ya neno asilia na neno linalokopwa. Kwa kutumia mwelekeo huu, makala yanaonyesha kwamba mbinu zinazotumiwa kwa maneno yanayokopeshwa ni pamoja na udondoshaji, udumishaji, ubadilishaji pamoja na uhamishaji wa konsonanti. Kwa upande mwingine, mbinu za utohozi zinazotumiwa kwa irabu ni kama vile uchopekaji, udumishaji na ubadilishaji. Mbinu hizi huhakikisha kuwa maneno mkopo yanashabihiana kwa kiasi kikubwa na yale asilia ya Kiswahili.

**Maneno Muhimui:** Ukopaji, maneno mkopo, utohozi, chanzo, ushabaha, kifonolojia, Kiswahili, Kikikuyu

## Utangulizi

Makala haya yanachunguza namna ambavyo maneno mkopo kutoka Kiswahili yanavyotoholewa kifonolojia ili yaweze kujitoshesha katika muundo wa lugha ya Kikikuyu. Kwa sasa, lugha ya Kikikuyu hutumiwa kwa mapana katika eneo la Kati la Mlima Kenya. Katika makala haya, lugha ya Kikikuyu inachukuliwa kuwa na lahaja tano, yaani Kimathira, Kindia, Kigichugu, Kikiambu (lahaja ya kusini) na Kimurang'a (lahaja ya Kaskasini) kama zinavyoelezwa na wasomi wa Kikikuyu kama vile Njoroge (1978), Gathenji (1981), Mutahi (1983), Wachera (2008) na Iribemwangi (2012, 2016). Mwelekeo wa Ushabaha-Chanzo wa utohozi wa manenomkopo ambao umetumiwa katika makala haya hujikita katika matumizi ya vikwazo maalumu vya uaminifu vya manenomkopo ambavyo hulazimisha kuwepo kwa mfanano mkubwa baina ya umbo la chanzi-wazwa na umbo mkopo linaloana na nalo.

Lugha ya Kikikuyu imekuwa na mtagusano wa muda mrefu na Kiswahili. Mtagusano huu ulianza hata kabla ya zama za ukoloni na kwa kiwango kikubwa unaendelea kutajirisha lugha ya Kikikuyu hasa kupitia kuingizwa kwa maneno ya kigeni. Langacker (1968: 176) anaeleza kwamba “kila lugha ambayo wazungumzaji wake wamewahi kutagusana na lugha nyingine haiwezi kuepuka maumbo mkopo asilani.”<sup>1</sup> Campbell (1988: 57) anaita maneno haya ya kigeni “manenomkopo” na mchakato ambao huyaingiza maneno hayo katika lugha ya pili anaita “ukopaji wa kiisimu.” Istilahi hizi mbili zitaigwa katika makala haya.

Kwa upande wake, Wardhaugh (1977) anaeleza kwamba ukopaji ni mbinu ya kuongeza vipashio vipya vya msamiati katika lugha. Mtumizi wa lugha fulani hukopa neno kutoka kwa mtumizi wa lugha nyingine kama hana neno lililo tayari kwa matumizi yake ili kurejelea kitu fulani. Kwa mfano, kwa mujibu wa Radford n.w. (1999), ni wazi kwamba masetla wa kwanza wa Marekani Kaskasini walikuwa na mtagusano na wakazi asilia ambao tayari walikuwa wamebuni majina ya mahali na vitu. Masetla hao basi walikopa majina ya mahali kama vile Massachusetts, Wisconsin, Michigan na Chicago kati ya mengine. Mbali na lugha kuopa maneno mengi, lugha zenyewe pia hukopesha maneno. Swali lililo muhimu kwa wanaisimu ni: kwa nini watumizi lugha fulani hukopa maneno kutoka kwa lugha nyinginezo? Kimsingi, watumizilugha hukopa maneno kutokana na sababu za kawaida kabisa: uhitaji/haja na hadhi/fahari. Ukopaji pia hutokana na athari za kigeni. Katika baadhi ya nyakati, utamaduni wa kigeni hujilazimisha kwa watumizi wa lugha tofauti. Langacker (1968: 178) anaeleza

---

<sup>1</sup> Tafsiri hii na nyinginezo zinazofuata ni zetu.

kwamba “uvamizi wa Uingereza na Wanorma mnamo 1066 uliingiza maneno mengi katika lugha ya Kiingereza.”

Ukopaji wa maneno ni jambo lisiloepukika baina ya lugha zinazotagusana. Katika kiwango cha fonolojia, utafiti kuhusu ukopaji husisimua pale ambapo lugha inayokopesha na ile inayokopa zina miundo ya kifonolojia inayotofautiana sana. Katika hali kama hizo, maneno hutoholewa na kuingia katika muundo wa lugha inayokopa. Hata hivyo, utohozi huo hukabiliwa na masharti fulani. Muhimu ni kwamba inaelekea kana kwamba kuna ulazima kwamba neno linalokopwa liweze kushabihiana na kwa namna ya ukaribu kabisa na neno asilia linalokopwa. Katika miaka ya karibuni, kumekuwa na tafiti nyingi za fonolojia zinazopendekeza mielekeo tofauti kuhusu ukopaji.

Katika utafiti wao kuhusu manenomkopo ya Kiingereza yaliyo katika Kifaransa cha Kananda, Poplack n.w. (1988: 64) wanahitimisha kwamba “jambo moja linalosababisha kuwepo kwa nominomkopo nyingi katika lugha ni ule uwezo wa nomino wa kujumuishwa kimuundo katika usemi wa lugha pokezi pamoja na hali yake ya kuwa kundi la maneno yabebayo habari za kileksika.” Nomino huwa wazi zaidi zikilinganishwa na aina nyingine za maneno. Moravasik (1978:11) anaeleza kwamba “ukopaji wa nomino ni jambo la kawaida katika lugha zinazotagusana. Lugha hukopa aina nyingine za leksika pale tu ambapo nomino zimekopwa mwanzo.”

#### **Yaliyoandikwa kuhusu Mada**

Katika maandishi, kuna kazi kadhaa kuhusu lugha ya Kikikuyu. Baadhi ya kazi za awali ni kama vile Barlow (1951) ambaye ameandika kuhusu sarufi fafanuzi ya Kikikuyu. Gechaga (1953) pia ametafitia sarufi ya Kikikuyu. Armstrong (1967) anachunguza toni katika nomino na vitenzi vya Kikikuyu. Ford (1974) naye anachunguza mifumo ya toni na kiimbo katika Kikikuyu. Katika miaka ya karibuni, Gathenji (1981) anachunguza mofolojia ya vitenzi vya Kikikuyu kwa kutumia mwelekeo wa Sarufi Milisi. Kazi ya Mũgane (1997) ni nyingine fafanuzi na ambayo inachanganua sarufi ya Kikikuyu. Katika utafiti huu, Mugane anachanganua vipashio tofaututofauti vya Kikikuyu haswa virai nomino na aina za sentensi. Kazi ya Mwihaki (1998) inahusu ukopaji katika Kikikuyu. Hata hivyo, kazi hii inahusu maneno ambayo yamekopwa kutoka kwa Kiingereza (lugha isiyo ya Kibantu) ilhali utafiti wetu unahusu maneno yaliyokopwa kutoka kwa Kiswahili. Ngugi (2008) amechunguza utohozi wa kifonolojia na kimofolojia wa manenomkopo ya Kiswahili yaliyokopwa kutoka lugha ya

Kiingereza. Ngugi alikita utafiti wake katika lahaja ya Kusini.<sup>2</sup> Iribemwangi (2012) anachunguza fonolojia ya lahaja za Kikikuyu huko akipendekeza uoanishaji wa fonolojia na othographia ya Kikikuyu, Kiambu na Kimbeere. Mwandishi anaainisha fonimu za lahaja mbalimbali za Kikikuyu na katika utafiti wa sasa, tunatumia uanishaji huu.

Iribemwangi (2010) anachunguza mabadiliko ya kisauti yanayotokea kwa manenomkopo katika lugha ya Kiswahili na kudadisi vile mabadiliko hayo yanavyoana na mofofonolojia ya Kiswahili. Kimani (2005) anachunguza utohozi wa maneno ya Kimaasai yanayokopwa na Kikikuyu. Anachunguza namna maneno hayo yanavyobadilishwa na hasa anajikita katika michakato iliyotokea pamoja na athari zake katika fonolojia na/au mofolojia ya Kikikuyu. Mberia (1993) anachunguza mabadiliko yanayotokea katika manenomkopo ya lugha ya Kitharaka. Chege (2009) katika utafiti kuhusu namna ambavyo manenomkopo hutoholewa katika lugha ya Kimaasai anatumia Nadharia ya Vikwazo na Mbinu za Urekebishaji (*Theory of Constraints and Repair Strategy*). Nadharia hii inafanana sana na mwelekeo wa Mshabaha-Chanzo tunaoutumia katika utafiti huu. Amechunguza manenomkopo ya Kimaasai yenye asili ya Kiingereza na Kiswahili.

Katika kazi yao kuhusu udumishaji na mabadiliko finyu katika utohozi wa manenomkopo, Paradis and Lacharite (1997) walichunguza manenomkopo ya Kifaransa katika lugha ya Kifula inayozungumzwa Afrika Magharibi. Walikusudia kudhihirisha kwamba utohozi wa kipandesauti, uhifadhi na udondoshaji na mambo yanoyoweza kutabirika katika ukopaji. Katika uchunguzi wao huo, walitumia Nadharia ya Vikwazo na Mbinu za Urekebishaji ambayo hukubalika na kutumika kwa kiasi kikubwa katika mwelekeo wa Mshabaha-Chanzo.

Kayiegema (2010) anachunguza maswala ya kimofolojia na kisemantiki ya manenomkopo ya Kinyarwanda kutoka kwa Kifaransa na Kiingereza. Utafiti huu unachunguza ni vipi, kwa nini na kwa kiasi kipi manenomkopo kutoka Kifaransa na Kiingereza yametoholewa ili kupatana na ngeli za nomino za Kinyarwanda. Kwa upande wake, McManus (2008) anachunguza manenomkopo ya Kiingereza katika lugha asili kadhaa za Australia. Katika utafiti wake, McManus anatumia mwelekeo wa Mshabaha-Chanzo wa Utohozi wa Manenomkopo sawa na utafiti huu unavyofanya.

---

<sup>2</sup> Kwa maelezo kuhusu aina tofautitofauti za lahaja za Kikikuyu, tazama Mutahi (1983) na Wachera (2008).

---

Katika kuchanganua lugha ya Kikantonisi, Silverman (1992) anaonyesha namna ambavyo fonolojia ya manenomkopo ilivyo na ngazi mbili bayana: ngazi ya kimawazo na ngazi ya kiutendaji. Arlotto (1972:184) anaeleza kwamba “ukopaji wa maneno kamilifu ndiwo mtagusano unaoenea sana baina ya lugha.” Anatoa pia sababu za ukopaji, kwa mfano, ukopaji wa vifaa vya kitamaduni. Kifaa kama hicho kinapokopwa, huingizwa katika jamii pamoja na neno linalotumiwa kukitajia katika lugha inayochangia.

### **Misingi ya Kinadharia: Mshabaha-Chanzo wa Utohozi wa Manenomkopo**

Ili kuelewa namna ambavyo manenomkopo hutoholewa katika lugha, utafiti huu unatumia mwelekeo wa Mshabaha-Chanzo wa Utohozi wa Manenomkopo (Smith, 2009). Mwelekeo huu huchunguza uaminifu wa manenomkopo kwa vikwazo ambavyo hushurutisha kuwepo kwa mshabaha mkubwa baina ya umbo-wazwa na nenomkopo halisi linalotamkwa. Mwelekeo huu unasisitiza kuwepo kwa ukaribu baina ya umbo-wazwa asili na umbo haswa linalotamkwa.

Mwelekeo wa Smith (2009) unaeleza kwamba katika fonolojia ya lugha, kuna ulinganifu baina ya umbo ndani la kimawazo na umbo nje linalotamkwa. Smith anaeleza kwamba umbo-wazwa huwa si umbo-ndani la ama la lugha kopwa au la lugha kopa; ni umbo dhahania la kimawazo tu. Hata hivyo, mshabaha-mkopo huhakikisha kuwa umbo-tamkwa la nenomkopo huwa aminifu kwa umbo-wazwa kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo. Mwelekeo huu hukubali kuwepo kwa ulinganifu-wazwa katika uteuzi wa mbinu za utohozi (Yip, 2002; Kang, 2003) na hukubali pia kudondoshwa kwa vipashio visivyo vikuu katika kiwango cha udhahania - yaani cha kabla ya ufonolojia (Peperkamp na Dupoux, 2003; Yip, 2002; Shinohara, 2006). Katika kuhitimisha swala la ukopaji, Arlotto (1972: 184) anaeleza hoja moja muhimu sana kuhusu ukopaji; anasema kuwa “maneno yanayokopwa husilimishwa katika muundo wa kifonemiki (au kisauti) wa lugha inayokopa.”<sup>3</sup> Hii inamaanisha kuwa neno likisha ingia kabisa kwenye lugha mpya, neno hilo husikika kama neno la kawaida la lugha hiyo na hubanwa na sharia na taratibu zote za lugha hiyo. Kutokana na yote tuliyoyasema hapo juu, nenomkopo basi ni neno linalotolewa kwa lugha tofauti na kutoholewa katika umbo lake la kifonemiki, tahajia, uwanja au maana kwa kufuatia msingi wa lugha pokezi.

---

<sup>3</sup> Baada ya kusema hayo, ni muhimu kutaja kwamba nyakati nyingine lugha huweza kuchukua fonimu (sauti) mpya kupitia kwa mtagusano wa lugha japo tukio hili huwa nadra. Sauti za kidoko, kwa mfano, ziliingia katika lugha za Kibantu za kusini kutokana na mtagusano na lugha za Khoisan. Tazama Iribemwangi (2010: 179) kwa maelezo zaidi.

Kwa kuwa Kiswahili na Kikikuyu ni lugha zenye chimbuko moja la Kibantu, si rahisi kuelewa kama vipashio fulani vya kileksika vinafanana kutokana na ukopaji au usuli wake. Ili kukabiliana na swala hili, makala haya yanatumia data ambayo inawakilisha vitu vya kigeni kwa Kikikuyu. Baadhi ya vitu huenda vilikuwa vya kigeni pia kwa lugha ya Kiswahili lakini kama vina asili ya lugha kama vile Kiarabu, Kiajemi, Kituruki, Kihindi au Kireno, basi ni salama kuchukulia kwamba maneno hayo yamekopwa kutoka Kiswahili. Hii ni kwa kuwa Kiswahili kilitagusana na lugha hizi miaka mingi kabla ya Kikikuyu. Mifano ya maneno ya aina hii ni kama vile /baha□a/ - /mbaha□a/ (bahasha, Kituruki); /meza/ - /mεΔa/ (meza, Kireno); /balɔzi/ - /faroΔi/ (Balozi, Kituruki); /baNgili- /faNgiri / / (bangili, Kihindi); /karata/ - /karata/ (karata, Kireno) na /alhamisi/ - /aramiΔi/ (alhamisi, Kiarabu) kati ya mengine mengi. Mananeno haya yanaashiria hali ya mkopo usiokuwa wa moja kwa moja. Katika hali hii, Kikikuyu kimekopa maneno haya kutoka kwa Kiswahili. Inaelewaka pia kwamba lugha za Kiswahili na Kikikuyu zimekuwa na mtagusano wa muda mrefu. Kigezo kingine ambacho kimetumiwa katika utafiti huu ni kile cha kimazingira. Manenomkopo ya vifaa vinavyopatikana na kutumiwa katika mazingira ya pwani kwa kawaida yamechukuliwa kuwa yana asili ya Kiswahili.

#### **Maelezo Mafupi kuhusu Fonolojia na Mofolojia ya Kikikuyu na Kiswahili**

Kikikuyu na Kiswahili ni lugha za Kibantu. Kutokana na unasaba huu, miundo ya lugha hizi inafanana sana. Hata hivyo, lugha hizi zina lahaja tofautitofauti na katika Kiswahili data ya makala itatoka kwa lahaja sanifu pekee ilhali lugha ya Kikikuyu itashughulikiwa katika ujumla wake.

#### **Fonolojia**

Lugha hizi mbili zina idadi tofauti ya irabu. Kiswahili kina irabu tano pekee ilhali Kikikuyu kina irabu saba. Juu ya hayo, kama anavyotaja Mutahi (1983), urefu au ufupi wa irabu ni sifa bainifu katika Kikikuyu, na kwa sababu hiyo kuna ubainishi kati ya irabu ndefu na fupi. Ukweli huu unapelekea kusema kuwa kiuamilifu Kikikuyu huwa na irabu kumi na nne. Ingawa urefu wa irabu mara nyingine hudhihirika katika Kiswahili, haujatambuliwa kama sifa bainishi muhimu na wanafonolojia wengi wa Kiswahili<sup>4</sup> kama ilivyo katika Kikikuyu. Irabu msingi tano za Kiswahili ni:

/i/ irabu ya mbele juu midomo isiyoviringwa

/u/ irabu ya nyuma juu midomo iliyoviringwa

---

<sup>4</sup> Kwa mjadala wenye kina kuhusu fonimu za Kiswahili kwa mujibu wa wanaisimu mbalimbali, tazama Iribemwangi (2008: 37-53)


/ɛ/ irabu ya mbele nusu-chini midomo isiyoviringwa

/ɔ/ irabu nyuma nusu-chini midomo iliyoviringwa

/a/ irabu ya nyuma (karibu na nyuma) chini midomo iliyoviringwa


Irabu msingi za Kiswahili huunda kile Matthews (1997:384) anachokiita “mfumo wa irabu wa pemetatu” na hivyo hudhihirika ifuatavyo:

**Mchoro wa I: Mfumo wa pemetatu wa irabu za Kiswahili**



Kwa upande mwingine, Kikikuyu kina mfumo wa irabu wa pembenne na irabu zake kumi na nne zinaweza kuwakilishwa ifuatavyo:

**Mchoro wa II: Mfumo wa pembenne wa irabu za Kikikuyu**



Kwa kutumia maneno, sifa za irabu ndefu na fupi zinaweza kuelezwa ifuatavyo:

/i/ irabu ya mbele juu midomo isiyoviringwa

/u/ irabu ya nyuma juu midomo iliyoviringwa

/e/ irabu ya mbele nusu- juu midomo isiyoviringwa

/o/ irabu ya nyuma nusu-juu midomo iliyoviringwa

/ɛ/ irabu ya mbele nusu-chini midomo isiyoviringwa

/ɔ/ irabu ya nyuma nusu-chini midomo iliyoviringwa

/a/ irabu ya mbele chini midomo isiyoviringwa

Iribemwangi (2012:24) anaeleza kwamba katika lugha ya Kikikuyu, “irabu ndefu na fupi huunda jozi za mlinganuofinyu.” Hii ni kuumaanisha kwamba sifa ya urefu au ufupi wa irabu huweza kusababisha tofauti ya maana irabu hizo zikitumiwa katika jozi. Anatoa mifano ya jozi kama hizo zinazoashiria mlinganuofinyu.

Kwa upande wa konsonanti, wakati Kiswahili kina fonimu zipatazo 26, Kikikuyu kina 18 pekee. Kwa hivyo kuna tofauti kubwa sana baina ya fonimu za konsonanti za lugha hizi mbili. Tofauti nyingine kubwa ni kwamba vizuiwa vyote vyenye mghuno (vipasuo na vizuiwa-vikwamizwa) hutangulizwa kwa nazali katika Kikikuyu ilhali katika Kiswahili utangulizi huu hutegemea maneno binafsi na hivyo hautokei kila mara. Kwa muhtasari, konsonanti za Kikikuyu zinaweza kuwakilishwa ifuatavyo:

**Jedwali la I: Fonimu za Konsonanti za lugha ya Kikikuyu**

MAHALI PA KUTAMKIA	Makundi kwa mujibu wa Namna ya Kutamka					
	VITATIZWA			SONORANTI		
	VIZUIWA		VIKWA MIZWA			
	VIPASUO	VIZUIWA-KWAMIZWA		NAZALI	KIMADENDE	VIYEYUSHO
Midomo miwili	/mb/		/β/*	/m/		/w/
Midomo-meno			/f/*			
Meno			/Δ/§			
Ufizi	/t/ /nd/		/s/* /z/§	/n/	/r/	
Kaakaa-ufizi			/Σ/*			
Kaakaa gumu		/□  /tΣ/*		/□/		/j/
Kaakaa laini	/k/ /Nγ/		/Φ/	/N/		
Glota			/h/§			
JUMLA	5	1	5	4	1	2 (18)

\* [f] na [β] ni alofoni za /f/

§ [Δ] na [z] ni alofoni za [Δ]

+ [tΣ], [Σ] na [s] ni alofoni za [Σ]

§ Fonimu /h/ haipo katika lahaja ya Kigichugu

(Kutoka Iribemwangi (2012:31))

Lugha ya Kiswahili ina konsonanti zipatazo 26. Matumizi ya neno “zipatazo” ni makusudi. Hii ni kwa kuwa swala la idadi ya fonimu za Kiswahili halina makubaliano kati ya wasomi. Baadhi kama vile Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kwamba Kiswahili kina konsonanti 23 (pasipo kuhesabu viyeyusho vyake viwili) ilhali wengine kama Massamba n.w (2004) wameorodhesha konsonanti 27. Njogu n.w (2006) wamebainisha konsonanti 27 na viyeyusho 2, na hivyo kuwa na jumla ya fonimu za Kiswahili 34. Mwaliwa (katika Iribemwangi 2017) anaeleza kuhusu konsonanti 4 zinazotanguliwa na nazali juu ya nazali 25. Iribemwangi (2010) anaeleza kwamba Kiswahili kina konsonanti 27



(ikiwa ni pamoja na viyeyusho 2). Hata hivyo, makala haya yanatumia konsonati zifuatazo 25 katika uchanganuzi wake:

### Jedwali la II: Fonimu za Konsonanti za lugha ya Kiswahili

MAHALI PA KUTAMKIA	Makundi kwa mujibu wa Namna ya Kutamka						
	VITATIZWA			SONORANTI			
	VIZUIWA		VIKWAMIZWA	NAZALI	LIKWIDI		
	VIPASUO	VIZUIWA- KWAMIZ WA			KITAMBAZA	KIMADENDE	VIYEYUSHO
Midomo miwili	/p/ /b/*			/m/			/w/
Midomo-meno			/f/ /v/				
Meno			/ɸ/ /Δ/				
Ufizi			/ɔ/				
Kaakaa-ufizi	/t/ /d/		/s/ /z/	/n/	/l/	/r/	
Kaakaa gumu		/±/ /φ/		/ɔ/			/j/
Kaakaa laini	/k/ /g/		/Φ/	/N/			
Glota			/h/				
JUMLA	6	2	9	4	1	1	2 (25)

\*Mahali popote penye sauti mbili, iliyo kushoto sighthuna ilhali ya pili ni ghuna.

Swala lingine la kifonolojia linalofafanuliwa katika makala haya linahusu migao ya silabi za Kikikuyu. Hili litawezesha kuelewa maumbo ya silabi yanayowezekeka katika lugha hii. Ingawa maswala kuhusu muundo wa silabi kama vile mwanzo, kiini na mwisho pamoja na yale yanayohusu uzito wa silabi (silabi nzito na nyepesi) yanaweza kuwa muhimu, si ya kimsingi katika kuendeleza mjadala unaolengwa katika utafiti huu.<sup>5</sup> Kwa sababu hiyo, Makala haya yanatoa migao ya silabi kama inavyoainishwa na Iribemwangi (2016). Mgao wa kwanza ni ule unaosemwa kuwa wa muundo wa silabi unaopendelewa; ule wa konsonanti-irabu (KI). Kama ilivyo katika lugha nyingi za Kibantu (na kwa hakika za ulimwengu), huu ndio muundo unaobainisha silabi nyingi za Kikikuyu. Huu ndio muundo unaopatikana katika maneno kama vile: /kerato/ - kiatu (KISKISKI), /kebereti/ - kiberiti (KISKISKI), /Nyamera/ - ngamia (KISKISKI) na /mokuhe/ - mfupi (KISKISKI).

Muundo mwingine ni ule wa K<sup>1/2</sup>II. Hapa, konsonanti tofautitofauti hutumiwa katika nafasi ya mwanzo na kisha kufuatwa na kiyeyusho na irabu. Kuna maneno

<sup>5</sup> Hata hivyo, ni muhimu kutaja kwamba Wachera (2008: 29-37) ameshughulikia swala la muundo na uzito wa silabi za lahaja mojawapo ya Kikikuyu kwa undani.

mengi yenye mgao huu kama vile: /mwēri/ - mwezi (K<sup>1/2</sup>II \$KI), /mbwē:/ - mbweha (K<sup>1/2</sup>II \$I), /orja/ - uliza (I\$ K<sup>1/2</sup>II). Katika migao hii, kimoja kati ya viyeyusho viwili vya Kikikuyu (/w/ au /j/) kimetumika katika nafasi ya kati. Lugha ya Kikikuyu pia huwa na silabi I. Hizi ni silabi zenye irabu moja na huwa nyingi. Hutokea katika nafasi yoyote ile katika maneno ya Kikikuyu. Mifano ni: /ando/ - watu (I\$KI) na /ao/ - wao (watu) (I\$). Mgao mwingine wa silabi ni ule wa konsonanti na mfuatano wa irabu mbili (KII). Kama ilivyokwishaajwa, urefu au ufupi wa irabu ni kigezo muhimu sana katika lugha ya Kikikuyu kwa kuwa huchangia maana moja kwa moja. Mgao huu hudhihirika katika maneno mengi sana, kwa mfano: /ta:ta/ - dondoka (KII\$KI), /Δa:ka/ - cheza (KII\$KI) na /ri:ka/ - rika (KII \$KI).

Kama inavyodhihirika, lugha ya Kikikuyu haina migao mingi ya silabi. Mgao wa KIKI unapendelewa sana katika lugha hii. Silabi wazi pia hutumika zaidi katika lugha hii ikilinganishwa na silabi funge ambazo hazipendelewi kabisa. Hata pale ambapo silabi funge zinapotokea kutokana na manenomkopo, ufunge huo hubatilishwa mara moja kupitia kwa mfanyiko wa uchopekaji wa irabu; kitendo ambacho huzua silabi zinazopendelewa.

Lugha ya Kiswahili kwa upande mwingine ina migao ya silabi isiyopungua tisa. Tofauti na Kikikuyu, Kiswahili kina silabi funge. Silabi hizi hutokana na mkopo. Kwa muhtasari, Iribemwangi (2010:54-58) anabainisha migao ifuatayo ya silabi za Kiswahili: konsonanti na irabu (KI); konsonanti mbili na irabu (KKI); konsonanti, kiyeyusho na irabu (K<sup>1/2</sup>II); konsonanti mbili, kiyeyusho na irabu (KK<sup>1/2</sup>II); silabi irabu (I); silabi konsonanti (K); konsonanti na Irabu mbili zikifuatana (KII); silabi funge na konsonanti tatu zikifuatwa na irabu moja (KKKI). Utafiti unadhihirisha kuwa mifanyiko miwili ya mwisho hapo juu inatokana na ukopaji.

### Mofolojia

Katika ngazi ya mofolojia, makala haya yanawasilisha ngeli-nomino za Mame-Bantu, Kikikuyu na Kiswahili. Uwasilishi huu utasaidia katika kubainisha michakato ya utohozi inayotokea katika maneno yanapokopwa kutoka Kiswahili hadi Kikikuyu. Uwasilishi utawezesha pia kulinganisha maumbo asili na maumbo mkopo kwa kurejelea maumbo mame. Ngeli za nomino za Mame-Bantu zilizo katika Jedwali la III hapa chini ziliainishwa mwanzo na Meinhof (1932:40). Meinhof aliorodhesha ngeli za nomino 21 tofauti na Guthrie ambaye alikuwa ameorodhesha ngeli 19. Jedwali la III limenakiliwa kutoka Miti (2006:113-114) japo kwa mabadiliko machache.

### Jedwali la III: Viambishi vya ngeli za nomino za Mame-Bantu, Kikikuyu na Kiswahili

Ngeli	Mame-Bantu	Kikikuyu	Kiswahili	Maelezo
1	*mu-	mo-	m-	umoja wa ngeli ya 2
2	*va-	a-/e-	wa-	wingi wa ngeli ya 1
3	*mu-	mo-	m-	umoja wa ngeli ya 4
4	*mi-	me	mi-	wingi wa ngeli ya 3 na wakati mwingine ya 14
5	*li-	i/ri	ji-	umoja wa ngeli ya 6
6	*ma-	ma-/mε	ma-	wingi wa ngeli ya 5 na ya 14
7	*ki-	ke-/ge-	ki-	umoja wa ngeli ya 8
8	*vi-	i-/cio-	vi-	wingi wa ngeli ya 7
9	*ni-	n-	N-	umoja wa ngeli ya 10
10	*li-/ni-	n-/m-	N-	wingi wa ngeli ya 9 na ya 11
11	*lu-	ro-	u-	umoja wa ngeli ya 10 na wakati mwingine ya 12
12	*tu-	ka - /ra	--	wingi wa ngeli ya 13, 19 na wakati mwingine ya 11
13	*ka-	to-	--	umoja wa ngeli ya 12 na wakati mwingine ya 14
14	*vu-	o-	u-	wakati mwingine umoja wa ngeli ya 4, 6 na wakati mwingine wingi wa ngeli ya 13
15	*ku-	ko-/go-	ku-	vitenzijina
16	*pa-	ha-	pa-, ni-	'kwa -', 'juu ya -'
17	*ku-	ko-	kwa-, ni-	'nje ya -'
18	*mu-	---	mwa-, ni-	'ndani ya -'
19	*pi-	---	---	umoja wa ngeli ya 12
20	*ɣu-	---	---	
21	*ɣi-	---	---	

Baada ya kueleza maswala hayo machache kuhusu ukopaji pamoja na fonolojia na mofolojia ya Kiswahili na Kikikuyu, makala haya sasa yataanza kuchanganua utohazi wa manenomkopo ya Kikikuyu yanayotoka kwa lugha ya Kiswahili.

#### Utohozi wa Manenomkopo ya Kikikuyu kutoka Kiswahili: Mjadala na Matokeo

Kwa kuwa Kiswahili ni lingua franka katika eneo ambamo Kikikuyu huzungumzwa, kuna maneno mengi ambayo yameingia kwenye Kikikuyu kwa sababu ya mtagusano wa lugha hizi mbili. Kule kupatana na Kiswahili huweza kuathiri wanaokopa kufananisha nenomkopo na lile asili kwa kiasi kikubwa. Jambo hili pia hutokana na uelewa wa sarufi na pia muundo wa kifonolojia na kimofolojia wa lugha inayokopesha (Kiswahili) na wanauwili/wanawingi lugha wa Kikikuyu.

Kama ilivyokwisha kutajwa, Mwelekeo wa Mshabaha-Chanzo wa Utohozi wa Manenomkopo husisitiza kuwepo na mfanano mkubwa baina ya umbo-wazwa na nenomkopo halisi linalotamkwa. Mwelekeo huu pia huhusisha moja kwa moja muundo wa neno asili na mbinu za utohazi zitakazotumiwa. Hivyo basi, muundo wa neno fulani Kiswahili unaweza kuhusishwa moja kwa moja na mbinu za

kifonolojia za utohozi kwa mujibu wa mwelekeo huu. Mbinu hizi huwezesha maumbo yanayokopwa kushabihiana kwa karibu na maumbo asili.

### Mbinu za Utohozi wa Konsonanti

Mbinu za utohozi wa maneno yanayokopwa na Kikikuyu kutoka kwa Kiswahili ambazo zimechanganuliwa katika makala haya ni udondoshi, udumishaji, ubadilishaji na uhamishaji.

### Udondoshaji wa konsonanti

Mshabaha wa kimawazo katika uteuzi wa mbinu ya utohozi (Yip, 2002; Kang, 2003) hukubali udondoshaji wa vipashio visivyo vikuu katika kiwango cha kimawazo. Mfanano huu ni muhimu sana katika uchanganuzi wowote unaotumia mwelekeo wa Mshabaha-Chanzo kwa kuwa umbo-wazwa huathiriwa na mawazo, othografia na mambo mengine ya fonolojia ya lugha husika.<sup>6</sup> Kigichugu ni lahaja mojawapo ya Kikikuyu inayozungumzwa katika kaunti ya Kirinyaga. Lahaja hii haina sauti kikwaruzo-mghuno cha glota /h/ katika fonimu zake. Hata hivyo, kama inavyodhihirika katika Jedwali la II, sauti hii inapatikana katika lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hiyo, fonimu /h/ ikitokea katika nenomkopo linaloingia katika lahaja hii, fonimu hiyo hudondolewa kwa kuwa haipatikani katika lahaja yenyewe. Udondoshaji huo hasa hutokea pale /h/ inapofuatiwa na irabu za chini (tazama Mchoro wa II) kama vile /a/ na /ε/ kama inavyothibitishwa kataka data (1) hapa chini:

(1)

<b>Kiswahili (A)</b> <sup>7</sup>	<b>Kikikuyu</b> <sup>8</sup> (M)	<b>Neno</b>
/kahawa/	/kaoa/	kahawa
/hεkalu/	/εkaro/	hekalu
/ðahabu/	/ða:βu/	dhahabu

Maneno haya matatu yanarejelea vitu ambavyo ni vya kigeni kwa wazungumzaji wa Kikikuyu. Maoni yetu ni kwamba vitu hivi ni vya kigeni pia

---

<sup>6</sup> Tazama mchoro na maelezo yanayofuata katika makala ya Smith, J. L. kuhusu Mwelekeo wa Mshabaha-Chanzo wa Utohozi wa Manenomkopo katika uk 3 kuendelea kwenye <http://www.unc.edu/~jlsmith/home/pdf/phonarg.pdf> (makala yalipitiwa Julai 18, 2018).

<sup>7</sup> (A) inawakilisha neno asili ilhali (M) inawakilisha nenomkopo

<sup>8</sup> Msisitizo hapa ni kwamba mfanyiko huu hudhihirika katika lahaja ya Kigichugu pekee. Lahaja nyingine za Kikikuyu zina fonimu /h/.

---

katika lugha ya Kiswahili lakini watumizi wa Kiswahili walitagusana nazo kabla ya watumizi wa Kikikuyu. Kwa sababu hiyo, ni salama kuamua kwamba Kiswahili ndiyo lugha changizi katika hali hii.

### Udumishaji wa Konsonanti

Pale penye vipandesauti vya Kiswahili vinavyoshabihiana na vile vinavyopatikana kwenye Kikikuyu, kwa kawaida vipandesauti hivyo hudumishwa katika manenomkopo. Kipandesauti hiki hudumishwa kama inavyodhihirika katika mifano 2 hadi 9:

(2)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/karata/	/karata/	karata
/karatasi/	/karataði/	karatasi
/kitamba:/	/ɣetambaja/	kitambaa

Fonimu ya Kiswahili /k/ hudumishwa kama ifuatavyo:

(3)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/kiatu/	/kerato/	kiatu
/kalamu/	/karamu/	kalamu
/duka/	/nduka/	duka

Fonimu ya Kiswahili /d/ hudumishwa<sup>9</sup> kama ifuatavyo:

(4)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/duka/	/nduka/	duka
/sanduku/	/iðandoko/	sanduku
/bendera/	/fendera/	bendera

---

<sup>9</sup> Kipasuo ghuna /d/ hutangulizwa na nazali /n/ ili kushabihiana na sauti ya karibu ya Kikikuyu, /nd/. Kama tulivyotaja, vizuiwa vyote ghuna katika lugha ya Kikikuyu hutangulizwa na nazali (tazama Jedwali la I).

Fonimu ya Kiswahili /m/ hudumishwa kama ifuatavyo:

(5)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/meza/	/mɛða/	meza
/mkate/	/moyate/	mkate
/msumari/	/moΣumare/	msumari

Katika lahaja za Kindia na Kigichugu za Kikikuyu /s/<sup>10</sup> hudumishwa ifuatavyo:<sup>11</sup>

(6)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/pesa/	/mbesa/	pesa
/alhamisi/	/aramisi/	alhamisi
/sindano/	/sindano/	sindano

Fonimu ya Kiswahili /ɲ/ hudumishwa kama ifuatavyo:

(7)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/ɲapa/	/ɲapa /	nyanya
/mɲapara/	/moɲafara/	mnyapara

Fonimu ya Kiswahili /r/ hudumishwa kama ifuatavyo:

(8)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/ɣari/	/Nɣari/	gari
/siri/	/ðiri/	siri
/barua/	/maroa/	barua

Fonimu ya Kiswahili /Σ/ hudumishwa katika baadhi ya lahaja za Kikikuyu kama ifuatavyo:

---

<sup>10</sup> Kama itakavyodhihirika katika data 12 wakati mwingine fonimu /s/ hubadilishwa na kikwamizwa-meno ghuna /ð/. Swala hili linajadiliwa zaidi baadaye.

<sup>11</sup> /s/ imeelezwa kama mojawapo ya alofoni za /Σ/ na kwa hivyo katika baadhi ya lahaja za Kikikuyu hujitokeza pia kama /Σ/ na pia /tΣ/ (tazama Jedwali la I).

---

(9)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/dirifa/	/ndirifa/	dirisha
/mafindano/	/mafindano/	mashindano
/bahafa/	/mbahafa/	bahasha

Udumishaji huu haujitokezi katika lahaja zote za Kikikuyu; katika lahaja za Kindia na Kigichugu mabadiliko hudhihirika kwa kuwa alofoni [s] hudhihirika mahali pa /Σ/.

Katika data 2 hadi 9 hapo juu, baadhi ya konsonanti zinazopatikana katika lugha za Kiswahili na Kikikuyu zinadumishwa katika manenomkopo. Udumishaji huu unahakikisha kwamba nenomkopo linasalia kufanana sana na neno asili hata pale ambapo baadhi ya fonimu nyingine zinabadilika.

#### Ubadilishaji wa Konsonanti

Imeelezwa katika Sehemu 1.4 kwamba Kiswahili kina konsonanti nyingi kuliko Kikikuyu.<sup>12</sup> Zile fonimu za Kiswahili ambazo hazipo katika Kikikuyu hubadilishwa na zile zinazokaribiana sana nazo kifonetiki. Jambo hili hutokana na ukweli kwamba watumizi wa Kikikuyu huziwaza fonimu hizo kama zile zinazofanana na zile zinazokopwa. Hili huwawezesha watumizi lugha kutamka maneno ambayo yana muundo sahihi kwa mujibu wa lugha yao. Kama inavyoelezwa katika data 10 hapa chini, kitambaza ghuna cha ufizi /l/ katika lugha ya Kiswahili hujitokeza kama kimadende ghuna cha ufizi /r/ katika lugha ya Kikikuyu. Lugha ya Kikikuyu haina sauti /l/ katika fonimu zake.

(10)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/kalamu/	/karamu/	kalamu
/suluali/	/ðuruare/	suluali
/pilipili/	/firifiri <sup>13</sup>	pilipili

Kikwamizwa ghuna cha ufizi /z/ katika lugha ya Kiswahili hujitokeza kama kikwamizwa ghuna cha meno /ð/ katika lugha ya Kikikuyu. Sababu ni kwamba

<sup>12</sup> Tazama Jedwali la I na la II kuona konsonanti zote za Kiswahili na Kikikuyu.

<sup>13</sup> Katika neno hili, sauti /p/ vilevile inabadilika na kuwa /f/. Huu ni uthoofikaji ambapo kizuiwa kinabadilika na kuwa kikwamizwa. Badiliko hili linatokea kwa kuwa lugha ya Kikikuyu haina fonimu /p/. Inayoikaribia kimatamshi ni /f/ kwa kuwa yenyewe pia ni [+ Anteria].

nyingi ya lahaja za Kikikuyu haina fonimu /z/<sup>14</sup>. Ni muhimu kuona kwamba /z/ na /ð/ ni fonimu za anteria zenye sifa ya mghuno. Data 11 hapa chini inawakilisha badiliko hili:

(11)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/meza/	/meða/	meza
/mzuNɣu/	/moðoNɣo/	Mzungu
/kijɔzi/	/kijnoði/	kinyozi

Vipasuo vya Kiswahili vya midomoni /p/ na /b/ hudhihirika kama /f/ (au alofoni yake [β]) katika Kikikuyu. Lugha ya Kikikuyu haina fonimu /p/ wala /b/. Kimawazo, fonimu inayokaribiana nazo ni /f/ ambayo pia ni ya anteria. Mifano ya badiliko hili inaonekana katika data 12 hapa chini.

(12)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/mabati/	/mafati/ na /maβati/	mabati
/bendera/	/fendera/ na /βendera/	bendera
/padri/	/fatere/ na /βatere/	padri
/paɣya/	/faɣya/ na /βaɣya/	paɣya

Katika baadhi ya nyakati, kikwamizwa cha ufizi kisoghuna /s/ huweza kujitokeza kama kikwamizwa ghuna cha meno /ð/ kama inavyodhihirika katika data 13 hapa chini:

(13)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/sabuni/	/ðafuni/	sabuni
/serikari/	/ðirikari/	serikali
/pasi/	/faði/	pasi
/supu/	/ðufu/	supu

Katika kuelezea data 6 hapo juu, ilielezwa kwamba wakati mwingine /s/ hudhihirika kama /s/, /Σ/ au /tΣ/ kutegemea lahaja inayohusika. Kubadilishwa kwa /s/ na /ð/ ni jambo linalokanganya kwa sababu mbili. Kwanza, kwa kufuatia mwelekeo unaoongoza uchunguzi huu, sauti ambazo hubadilishwa ni zile ambazo hazipo katika mfumo wa sauti wa lugha pokezi. Hata hivyo, fonimu /s/ (ama

---

<sup>14</sup> Lahaja ya Kimathira ina fonimu /z/. Katika lahaja hiyo, sauti /z/ **hudumishwa** katika manenomkopo.

---



alofoni zinazohusiano nayo) imo katika lugha ya Kikikuyu. Kwa sababu hiyo, haionekani kama kuna sababu yoyote muhimu inayolazimisha kuwepo kwa badiliko hilo. Sababu ya pekee inayoweza kushawishi badiliko hili ni mfanyiko wa kifonolojia. Wazo hili linatuingiza kwenye sababu ya pili; kwamba ubadilishaji huu hauonekani kuchochewa na mfanyiko wowote wa kifonolojia. Hii ni kwa kuwa japo sauti hizo mbili zinatokea katika mazingira tofauti, mazingira hayo yanafanana kwa kuwa zinatanguliwa au kufuatiwa na fonimu tofautitofauti; irabu (za juu, chini, kati, mbele na nyuma) katika ujirani wa konsonanti tofauti (nazali, vizuiwa vilivyotangulizwa na nazali, ghuna na zisizoghuna, za anteria na zisizo na anteria, za korona na zisizo za korona nk). Jambo hili linahitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

Kipasuo ghuna cha kaaka laini cha Kiswahili /ɣ/ hudhihirika kama kikwamizwa ghuna cha kaaka laini /ɣ/ katika Kikikuyu. Kikikuyu hakina fonimu /ɣ/ na /ɣ/ ndiyo fonimu inayoshabihiana nayo kimawazo na kimatamshi.

(14)

Kiswahili (A)	Kikikuyu (M)	Neno
/mɣɔmɔ/	/moɣɔmɔ/	mgomo
/ɣɔiɣɔi/	/ɣɔiɣɔi /	goigoi

### Uhamishaji wa Maneno

Wakati mwingine, lugha huwa na umbomkopo linalofanana moja kwa moja na umbo asili. Maumbo haya huweza kuwa kuchukua vipandesauti au hata miundo silabi isiyokuwa katika mfumo wa lugha pokezi. Aghalabu, huwa hakuna sababu mahsusi za kifonolojia au kifonetiki zinazochochea kutokea kwa uhamishaji. Baadhi ya maumbo ya Kiswahili huhamishwa kwa Kikikuyu na kutamkwa kwa namna ileile kutokana na kuwa na mfumo sawa wa kiothografia. Data 15 hapa chini inaashiria uhamishaji wa maneno kutoka Kiswahili hadi Kikikuyu:

(15)

Kiswahili (A)	Kikikuyu (M)	Neno
/ɲaɲa/	/ɲaɲa/	nyanya
/ɲaɲana/	/ɲaɲana/	ng'ang'ana
/ndɔ:/	/ndɔ:/	ndoo

### Mbinu za Utohozi wa Irabu

Makala haya yanachanganua mbinu nne za utohozi wa irabu wa manenomkopo kutoka Kiswahili. Mbinu hizi ni uchopekaji-tena, uchopekaji, udumishaji na ubadilishaji.

### *Uchopekaji-tena<sup>15</sup> wa irabu*

Katika Jedwali la III imeonyeshwa kwamba wakati ambapo Kiswahili kina {m-} kama kiambishi cha ngeli ya 1 na ya 3, Kikikuyu na Mame-Bantu zina viambishi {mo-} na {mu-} mtawalia kwa ngeli nomino iyo hiyo. Kikikuyu kikikopa maneno yaliyo katika ngeli hizo, na ambapo {m-} inafuatwa na konsonanti, irabu /o/ huchopekwa tena. Kutokana na uchopekaji huo, neno linapata muundo unaokubalika katika lugha ya Kikikuyu wa KI. Muundo wa KKI si wa kawaida katika Kikikuyu. Makala haya yanatumia istilahi ya *uchopekaji-tena wa irabu* kwa kuwa ni dhahiri kuwa lugha ya Kiswahili ilipoteza irabu ya Mame-Bantu ambayo hufuata nazali ya midomo. Uchopekaji-tena huwezesha nenomkopo kuingia katika ngeli nomino ifaayo ya lugha ya Kikikuyu. Mifano ni kama ifuatayo katika data 16:

(16)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/mpira/	/mofira/	mpira
/mkate/	/mɔvate/	mkate
/mkebe/	/mokefe/	mkebe
/mhindi/	/mohende/	Mhindi

### **Uchopekaji wa Irabu**

Kwa kawaida, irabu huchopekwa pale ambapo muundo wa silabi haukubaliki baada ya ukopaji. Uchopekaji huu huzua muundo wa silabi unaopendelewa. Hata hivyo, utohozi wa aina hii hautokei sana kwa kuwa lugha mbili hizi ni za Kibantu, zenye ukuruba na zinazotumia KIKI kama muundo unaopendelewa zaidi wa silabi. Mifano kuhusu uchopekaji wa irabu ni kama vile:

(17)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/alhamisi/	/aramiΔi/	Alhamisi
/dafraɔ/	/ndafurao/	dafrao

### **Udumishaji**

Kama inavyodhihirika katika Mchoro wa I Kiswahili kina irabu tano: /i/ /a/ /ɔ/ /u/ /a/ na /ɛ/. Aghalabu, irabu hizi hudumishwa katika manenomkopo. Mifano iliyo

---

<sup>15</sup> Ni uchopekaji-tena kwa sababu irabu yenyewe ipo katika leksika ya Mame-Bantu, inadondolewa katika Kiswahili na kisha kuchopekwa kwenye Kikikuyu baada ya kukopa neno.

---

katika 18 hapa chini inaonyesha udumishaji wa irabu tofautitofauti hasa irabu hizo zikitokea katika nafasi ya mwisho ya neno.

(18)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/sɔma/	/ðɔma/	soma
/siri/	/ðiri/	siri
/kijikɔ/	/ɾeΣikɔ/	kijiko
/petɛ/	/mbetɛ/	pete

### Ubadilishaji wa Irabu

Baadhi ya nyakati, irabu ya juu-nyuma - /u/ - ya Kiswahili huweza kudhihirika kama irabu ya kati-juu /o/ ya Kikikuyu katika manenomkopo kama katika mifano ifuatayo katika data 19:

(19)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/kifaru/	/kefaro/	kifaru
/barua/	/maroa/	barua
/mulika/	/moreka/	mulika

Katika hali hii, irabu ya juu hushushwa. Mchakato kama huu unaonekana katika data 20 hapa chini ambapo irabu ya Kiswahili ya mbele juu /i/ hudhihirika kama irabu ya nusu juu /e/:

(20)

<b>Kiswahili (A)</b>	<b>Kikikuyu (M)</b>	<b>Neno</b>
/kiti/	/vete/	kiti
/kalia/	/ikarera/	kalia
/kifaru/	/kefaro/	kifaru
/mulika/	/moreka/	mulika

Mifanyiko mingi ya irabu haielekei kuchochewa na sababu mahsusi za kifonetiki au za kifonolojia. Hata hivyo, inatambuliwa kwamba kwa kuwa lugha Kikikuyu ina irabu nyingi kuliko Kiswahili; kuna uwezekano kuwa mifanyiko fulani kama vile ubadilishaji ni jaribio la kuwa na irabu anuwai katika manenomkopo.

### Hitimisho

Makala haya yameonyesha kwamba Kiswahili huwa lugha changizi na kwamba imekopesha maneno mengi kwa lugha ya Kikikuyu. Katika kukopesha huko, maneno ambayo yanaingia katika lugha ya Kikikuyu hutoholewa ili kuchukua muundo wa lugha pokezi. Utohozi huo huhuzu fonimu za konsonanti na pia za irabu pia. Katika kutohoa konsonanti, mbinu zinazotumika ni pamoja na udondoshaji, udumishaji na ubadilishaji wa konsonanti tofautitofauti. Irabu

hutoholewa kwa kwa kutumia uchopekaji-tena, ubadilishaji na pia uchopekaji. Uhamishaji huhusu kuhamishwa kwa maneno kamili kutoka kwa lugha ya Kiswahili hadi Kikikuyu. Hata hivyo, imedhihirika kwamba hata yanapotoholewa, maneno haya hufanya hivyo kwa namna ambayo huachwa yakishabihiana sana na yale asili.

### Marejeleo

- Antilla, R. (1972). *An introduction to historical and comparative linguistics*. New York: Macmillan.
- Armstrong, L. (1967). *The phonetic and tonal structure of Kikuyu*. London: Dowson of Pall Mall.
- Barlow, A. R. (1951). *Studies in Kikuyu grammar and idiom*. Edinburgh: Blackwood & Sons.
- Chacha, M. (2009). "The adaptation of Swahili loanwords from Arabic: A constraint – based analysis". *The Journal of Pan African Studies* Vol. 2, no. 8.
- Chege, S. N. (2009). "Morphonological modifications of English and Kiswahili loanwords in Maasai." *Tasnifu ya Uzamili ambayo haijchapishwa*, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Dupoux, E. Kakehi, K, Y. Pallier, na Mealer, J. (1999). "Epenthetic vowels in Japanese: A perceptual illusion?" *Journal of Experimental Psychology. Human Perception and Performance* Vol. 25: kr 1568 – 1578.
- Fleischhacker, H. (2002). *Cluster dependent epenthesis asymmetries*. Mswada, U.C.L.A.
- Ford, K. C. (1974). *Tone and intonation in Kikuyu*, Ripoti ya utafiti ambayo haijchapishwa, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Gathenji, H. W. (1981). *Morphology of verbal extensions in Gikuyu*, Tasnifu ya Uzamili ambayo haijchapishwa, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Iribemwangi, P. I. (2017). "Analytical Issues in Standard Kiswahili Phonology" *Reyono Journal of Interdisciplinary Studies*. St. Thomas College, Kozhencherry, India. Vol. 6, No. 1, kr 52-68.
- Iribemwangi, P. I. (2016). "Kikuyu Phonology and Orthography: Any hope for continuity of indigenous languages?" katika Devy, G. N, G. V. Davis na K. K. Chakravarty. *The Language Loss of the Indigenous*, Oxon: Routledge. Kr 239-253.
- Iribemwangi, P. I. (2012). "A Case for the harmonization of Kikuyu, Kiembu and Kimbeere phonology and orthography" katika Ogechi N. O., J. A. Ngala & P. Iribemwangi (wah): *The harmonization and Standardization of Kenyan languages: Orthography and other aspects*. Cape Town: Centre for Advanced Study of African Societies (CASAS), Sura ya 2, kr 20-38.
- Iribemwangi, P. I. (2010). *The structure of Kiswahili: Sounds, sound changes and words*. Saarbrucken: VDM Verlag.
- Iribemwangi, P. I. (2008). "A synchronic segmental morphophonology of standard Kiswahili", *Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijchapishwa*, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

- Iribemwangi, P.I & D. W. Karuru (2012). "Phonological Adaptation of Kiswahili Loanwords in Gĩ-Gĩchũgũ Dialect of Gĩkũyũ Language: An Application of Source - Similarity Model" *Baraton Interdisciplinary Research Journal (BIRJ)*. Eldoret: Baraton University Press. Vol. 2 No. 2, kr 49-62.
- Kang, Y. (2003). "Perceptual similarity in loanword adaptation. English postvocalic word-final stops in Korean." *Phonology* No. 20, kr 219 – 273.
- Katamba, F. (1989). *An introduction to phonology*. London: Longman.
- Karuru, D. W. (2012). "Phonological and morphological adaptation of loanwords in Gĩ-Gĩchũgũ: An application of source - similarity model". *Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa*, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kenstowicz, M. (2003). "Salience and similarity in loanword adaptation: A case study from Fijian". *Language Sciences*, 29 (2007) kr 316- 340
- Kenstowicz, M. (2001/4). "The role of perception in loanword phonology". *Linguistique Africaine 20 and Studies in African linguistics*, 32, kr 95 -112.
- Kenstowicz, M. na Suchato, A. (2006). "Issues in loanword adaptation: A case study from Thai". *Lingua*, 116, kr 921 - 949.
- Kioko, A. N., M., Njoroge, na Kuria, P. (2012). "Harmonizing the orthography Gĩkũyũ and Kĩkamba" *katika Ogechi N. O., J. A. Ngala & P. Iribemwangi (wah): The Harmonization and Standardization of Kenyan Languages: Orthography and Other Aspects*. Cape Town: Centre for Advanced Study of African Societies (CASAS), Sura ya 3, kr 39-63.
- Lacharite, D. na Paradis, C. (2005). "Category preservation and proximity versus phonetic approximation in loanword adaptation". *Linguistic Inquiry*, 36, kr 223 – 258.
- Louriz, N. [www.essex.ac.uk/linguistics/publications/egsp/vol-6](http://www.essex.ac.uk/linguistics/publications/egsp/vol-6) makala yalipitiwa Mei 10, 2012.
- Mberia, K. (1993). "Kitharaka segmental morphology with special reference to the noun and the verb". *Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa*, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- McManus, H. E. (2008). "Loanword adaptation: A study of some Australian aboriginal languages" *Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa*, Sydney: Chuo Kikuu cha Sydney.
- Meinhof, C. & van Warundo, N.J. (1932). *Introduction to the Phonology of the Bantu Languages*. Berlin: Dietrich Reimer Ernst Vohsen.
- Miti, L. (2006). *Comparative Bantu phonology and morphology*. Cape Town: Centre for Advanced Study of African Societies.
- Mugane, J. M. (1997). *A paradigmatic grammar of Gĩkũyũ*. Stanford: CLSI Publications.
- Mutahi, K. E. (1983). *Sound change and classification of the dialects of Southern Mt. Kenya*. Berlin: Dietrich Reimer Verlag.
- Mwaliwa, H. C. (2014). "An Analysis of the Syllable Structure of Standard Kiswahili Loanwords from Modern Standard Arabic." *Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa*, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

- Mwihaki, A. N. (1998). "Loanword nativization: A generative view of the phonological adaptation of Gikuyu Loan Words." *Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijchapishwa*, Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Ngugi, G. K. (2008). "Phonological and morphological adaptation of English loanwords into the Kikabete dialect of Gikuyu language". *Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijchapishwa*, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Njoroge, D. (1978). "Kikuyu deverbatives and other nominalizations." *Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijchapishwa*, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Paradis, C. & D. Lacharite (1997). "Preservation and minimality in loanword adaptation". *Journals of Linguistic*, 33, kr 379 – 430.
- Peperkamp, S. (2004). "A psycholinguistic theory of loanword adaptations". Katika M. Ettliger N. Fleisher and M. Park-Doob (wah). *Proceedings on BLS*, 30, Berkeley, BLS. Kr 34 - 352.
- Peperkamp, S. & Dupoux, E. (2003). "Reinterpreting loanword adaptations: The role of perception," *Proceedings of the 15<sup>th</sup> International Congress of Phonetic Sciences*, kr 367 - 370.
- Prince, A. & Smolensky, P. (1993 / 2004). *Optimality theory: Constraint interaction in generative grammar*. Malden, MA: Blackwell.
- Silverman, D. (1992). "Multiple scansion in loanword phonology: Evidence from Cantonese" *Phonology*, 9, kr 289 – 328.
- Smith, J. L. (2009). "Source – Similarity in loan adaptation: Correspondence theory and the posited source – language representation". katika Steve Parker (mh.), *Phonological Argumentation Essays on Evidence and Motivation*. London: Equinox.
- Smith, J. L. (2006). "Loan phonology is not all perception. Evidence from Japanese loan doublets", Katika T. J. Vance na K. A. Jones (wah). *Japanese / Korean Linguistics*, 14, Stanford: CSLI. Kr 63 – 74.
- Steriade, D. (2001). "Directional asymmetries in place assimilation: A perceptual account" – katika E. Hume na K. Johnson (wah). *The Role of Speech Perception in Phonology*, New York: Academic Press. Kr 219 – 250.
- Wachera, S. K. (2008). "Tone as a distinctive feature in the lexicon of Gĩ-Gĩchũgũ dialect, Gĩkũyũ Language". *Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijchapishwa*, Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Werker, J. F. na Tees, R. C. (1984). "Cross – language speech perception: Evidence for perceptual reorganization during the first year of life". *Infant Behaviour and Development*, 7, kr 49 – 63.
- Yip, M. (2002). "Perceptual influences in Cantonese loanword phonology". Katika Kubonzo, H. (mh). *Aspects of loanword phonology. Journal of the Phonetic Society in Japan*.